



Mtakatifu Josemaría Escrivá

Mwanzilishi wa Opus Dei

SALA

Ee Mungu, kwa maombezi ya Bikira Maria Mtakatifu, ulimjalia padri wako Mtakatifu Josemaría neema nyingi zisizohesabika, ukamchagua kuwa mtume wako mwaminifu kupindukia ili aanzishe Opus Dei, njia ya kujitakasa katika kazi za kila siku na katika kutimiza wajibu wa kawaida wa Mkristu. Nisaidie mimi pia ili nami niweze kuyafanya mambo yote ya maisha yangu yawe nafasi ya kukupenda na kulitumikia Kanisa, Baba Mtakatifu na watu wote kwa furaha na moyo mwepesi, nikiangaza njia zote duniani kwa mwanga wa imani na upendo. Kwa maombezi yake Mtakatifu Josemaría, nijalie msaada ninaokuomba (taja ombi lako hapa). Amina.

Baba yetu. Salamu Maria. Atukuzwe Baba.

Popote pale yalipo matamano yako, kazi yako, mapenzi yako hapo ndipo pahali pako hasa pa kukutana na Kristu kila siku. Ni katika mambo ya kawaida, ya kiulimwengu, ambapo inatupasa kujitakasa, tukimtumikia Mungu na watu wote. Wanangu, kwenye upeo wa macho huonekana kama kwamba mbingu na ardhi huungana. Walakini pale hasa zinapoungana ni mioyoni yenu, mnapoyatakasa maisha yenu ya kila siku. (Mahubiri ya Mtakatifu Josemaría Escrivá, yaliyokuwa kuhusu kuupenda ulimwengu kwa dhati, aliyoyatoa Oktoba 8, 1967).

Mtakatifu Josemaría Escrivá alizaliwa mjini Barbastro, Uhispania, mnamo tarehe 9 Januari, 1902. Alipata sakramenti ya upadri tarehe 28 Machi, 1925 mjini Saragosa. Kwa mwongozo wa Mungu, tarehe 2 Oktoba 1928, aliianzisha Opus Dei. Tarehe 26 Juni, 1975, alifariki ghafla mjini Roma chumbani mle alimozoea kufanya kazi yake, baada ya kuitazama kwa upendo picha ya Mama yetu, Maria. Hadi wakati huo, Opus Dei ilikuwa imekwisha sambaa katika mabara yote matano ya ulimwengu, ikiwa na wanachama zaidi ya 60,000 kutoka mataifa 80, wanaolitumikia kanisa kwa moyo mmoja, wakijiunga kikamilifu na Baba Mtakatifu pamoja na Maaskofu, kama ilivyokuwa desturi yake Mtakatifu Josemaría. Baba Mtakatifu John Paul II alimtangaza mwanzilishi wa Opus Dei kuwa Mtakatifu tarehe 6 Oktoba, 2002 mjini Roma. Sikukuu yake inasherehekewa tarehe 26 Juni. Mwili wa Mtakatifu Josemaría umelazwa katika kanisa kuu la Prelature la Opus Dei liitwalo Malkia wa Amani, katika barabara ya Bruno Buozzi 75, mjini Roma.

Maelezo zaidi kuhusu Mtakatifu Josemaría Escrivá yanaweza kupatikana kwenye mtandao wa www.opusdei.or.ke na www.escrivaworks.org

Wanaojaliwa misaada kupitia kwa maombezi ya Mtakatifu Josemaría Escrivá wanaombwa kuliarifu Prelature la Opus Dei kupitia, kwa ofisi la Uchunguzi wa Watakatifu, Sanduku la Posta, 19884-00100 Nairobi, Kenya au Barua pepe: info.ke@opusdei.org

SWAHILI

Imeidhinishwa na Kanisa.